

Maswali

1. Lulu inatengenezwa namna gani?
2. Nini ilifanya lulu ikakuwa ya thamani kuu?
3. Lulu inafananiswa na nini?
4. Mfanyi biashara anafananishwa na nani?
5. Mfanyi biashara alifanya nini kupata lulu?
6. Tuige mfano gani?

Majibu

1. Lulu inatengenezwa kutoka kwa jiwe linalopatikana kwa mnyama wa majini.
2. Hii lulu ilikuwa mzuri zaidi tena kubwa.
3. Lulu ilifananiswa na Ufalme wa Mungu.
4. Mfanyi biashara anafananishwa na watu tofauti, waume na wake.
5. Aliuza kila kitu.
6. Tumuige Yesu. Alitoa uhai wake kwa ajili ya Ufalme.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



36 Lulu ya thamani kubwa

Marejeo

Mathayo 13:45—46

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba tunatakiwa tutambue Ufalme wa Mungu kwanza kabla ya chochote.

Maneno maalum

1. Mfanyi biashara + vitu vya thamani + miaka mingi
2. Tajiri + biashara
3. Vitu vya maana vilionekana
4. Lulu + kubwa + bora sana
5. Lulu moja + nzuri + hakuna bei
6. Alitaka kununua
7. Bei + mali yote + hakuna pesa
8. Uza yote + nunua lulu + furahi sana
9. Ufalme wa Mungu + ya thamana + wacha vyote
10. Yesu aliacha vyote + Mfalme wa Ulimwengu


36.1 Kulikuwa na mfanyi biashara aliyefanya biashara ya vitu vyat thamani kama mawe mazuri, johari na madini. Alikuwa na uzoevu wa hii biashara hata angejua bei ya kununua na kuuza dhahabu au fedha na kuamua bei papo hapo.

36.2 Nyumba yake ilikuwa kubwa na wafanyakazi wengi mno. Hakukuwa na haja ya yeze kuenda sokoni. Lakini alipenda kusafiri kwa soko tofauti kukutana na wenzake na kuangalia walivyokuwa wakiuza.

36.3 Alipokuwa akizunguka hivo angenunu vitu vizuri kama mkufu au bangili ya bintiye au kifungu cha mkewe au pete nzuri ya kidole cha mwanawewe atakapooa

36.4 Mawe yake mazuri yalikuwa lulu. Alipokuwa akisafiri bandarini, alitafuta kwa uangalifu lulu tu. Lulu ni aina ya mawe inayotoka kwa kiumbe fulani kipatikanaycho majini. Huwa inakua mpaka iwe kubwa na ni nzuri na ya thamani kubwa.

36.5 Alipokuwa kwa hiyo kazi yake, alikuta mfanyi biashara mwenzake na alikuwa amepata lulu kubwa na maridadi sana. Ilikuwa nyororo, nyeupe kama maziwa na haikukuwa na mkunjo wowote wala mawaa. Ilikuwa kubwa na ya mfaringo mzuri. Ilionekana lulu nzuri kwa zote zenye alizokuwa amepata.



36.6 Huyo mfanyi biashara alipoiona tualiitaka sana. Ilikuwa ya thamani zaidi ya maisha yake. Vyote alivyokuwa amepata vilikuwa bure akilinganisha na hii. Hakuitakia mke wala mtoto wake lakini yeze mwenyewe! Kama kuna kitu alichokitaka maishani mwake ilikuwa hii lulu.

36.7 Alipouliza mzee aliyekuwa akiuza bei yake, yule mzee alimwangalia sana. Alisema bei yenye huyo mfanyi biashara hajawahi kulipia kitu chochote maishani mwake. Hiyo Lulu ilikuwa inamkarimu utajiri wake wote na hangebaki na pesa yoyote akinunu. Lakini hiyo lulu ilikuwa nzuri sana lazima aichukue.

36.8 Alirudi nyumbani akaiza johari na mawe yote ya thamani na kumpelekea yule mzee. Akaichukuwa hiyo lulu nzuri akaiweka vizuri ili isichafuke wala kupotea au kuibwa. Kwa sasa alikuwa masikini sana lakini alikuwa amepata chenyeye moyo wake ultaka na alikuwa na furaha kuu.

36.9 Ufalme wa Mungu uko kama hiyo Lulu. Iko kama kitu tunachotaka kuliko vitu vyote. Tukitaka tuwe watu wa Ufalme, lazima tukubali kwamba tuwenye dhambi na tunatakiwa mwokozi. Lazima tutubu, tubebe msalaba na tumfuate Yesu. Hii ina maana kwamba tuache kila kitu cha dunia na tumfuate Yesu.

36.10 Yesu anataka tuwe kwa Ufalme wake. Anaangalia duniani kote aone waliotia neno moyone mwao na wawe wa haki. Na hata ametuba mfano mzuri alipojitolea kwa hali zote ili awe Mfalme kamili wa ulimwengu.